TANGAZO LA SERIKALI Na. 222 la tarehe 15/4/2022

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

(*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA USAFI WA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO ZA MWAKA, 2022

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo za mwaka 2022.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo au afisa yeyote aliyekasimishwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya mamlaka ya Halmashauri na ambaye ama ana kaya au anaishi

katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

Sura ya 191
"maji taka" maana yake ni ile iliyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191
"taka" maana yake ni ile iliyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191
"taka ngumu" Maana yake ni ile iliyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi anayemiliki eneo la nyumba,kiwanja au biashara kuhakikisha kwamba;-

(a) mazingira yanayozunguka eneo lake yanakuwa safi wakati wote;
(b) taka zote zinakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri;
(c) anachimba shimo la kutupia taka litakalokuwa na urefu usiopungua kimo cha futi 3 na upana usiopungua futi 2;
(d) anajenga choo imara cha kudumu kilichojengwa kwa matofali na kuezekwa kwa bati, tembe, majani, vigae chenye mlango unaofunga na kufunguka na kuhakikisha kwamba choo kinatumika wakati wote na kuwe na chombo cha maji tiririka na sabuni ya kunawa mikono;
(e) eneo lake halina mazalia ya mbu, panya na wadudu wengine hatarishi.

(2) Mtu yeyote atakaye kiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Uhifadhi wa maji taka

5.-(1) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara anatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa analo karo la kuhifadhi maji taka;
(b) kunyonya maji taka pale karo linapojaa; na
(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye

mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhia maji taka.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

6.-(1) Mtu yeyote anayetengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa:

(a) kutimiza masharti na kanuni za afya; na
(b) kuwa na kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri.

Upimaji wa afya

7. Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, migahawa, baa, nyumba za kulala wageni, bucha, waoka mikate, au watu wanaoshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa kuhakikisha kwamba wanapima afya zao kila baada ya miezi sita.

Uwezo wa afisa mwidhiniwa

8.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo kuingia katika eneo lolote ndani ya Halmashauri kabla ya saa 12:30 jioni ili kukagua mazingira.

(2) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuzuia watu au mtu kuishi katika jengo ambalo linahatarisha afya au maisha ya watu na viumbe hai.

Ada ya uzoaji taka

9. Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kutoka kwa kila kaya, wamilliki wa nyumba za biashara, taasisi na kampuni zilizopo ndani ya eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Eneo la kutupa taka

10.-(1) Halmashauri itawajabika -

(a) kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka;
(b) kuweka vyombo maalum vya kutunzia taka katika maeneo ya Halmashauri; na
(c) kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

Siku ya usafi

11.-(1) Kila jumamosi ya mwisho wa mwezi itakuwa ni siku maalamu ya kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi na umma.

(2) Itakuwa ni wajibu na lazima kwa kila mkazi katika kijiji na kitongoji kushiriki usafi wa mazingira kwa siku iliyopangwa na Halmashauri katika maeneo yao na maeneo ya umma.

Vikundi vya usafi

12. Halmashauri itahamasisha uundaji wa Vikundi Jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Marufuku

13. Itakuwa ni marufuku-

(a) mtu yeyote kuendesha biashara ya upulizaji dawa au biashara ya kuua wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni kutoka Halmashauri;

(b) mfugaji kuruhusu mifugo kuzurura hovyo mitaani au barabarani;

(c) mtu yeyote kutupa taka ovyo ndani ya eneo la Halmashauri;

(d) mtu yeyote kufungulia mziki kwa sauti ya juu ambayo itasababisha kelele na kuwa kero kwa wakazi wengine.

Makosa

14.-(1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote-

(a) kujenga choo chini ya umbali wa mita 60 kutoka kisimani, bwawani, mtoni, au chanzo kingine cha maji yanayotumika, kwa matumizi ya binadamu;

(b) kutoa kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, maji machafu, yenye kinyesi kutoka kwenye choo chake au bafu lake au karo la kuoshea vyombo au nguo au kutoka kwenye bomba lolote linalochukua maji machafu, na kuyatitirisha kwenye barabara, mitaa, au kwenye mifereji ya maji ya mvua, au mfereji wowote uliowazi;

(c) kutupa taka au kusababisha mtu mwingine atupe taka mahali popote palipokataliwa na Halmsahauri;
(d) kutiririsha maji machafu yanayoweza kusababisha kero kwa wakazi wa maeneo husika;
(e) kuuza chakula nje ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

Adhabu

15. Mtu yeyote anayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili jela au vyote kwa pamoja.

Kufililisha kosa

16. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi elfu thelathini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya kifungu cha 9*)

ADA YA KUZOA UCHAFU

SEHEMU A
ADA YA TAKATAKA KWA MWEZI.

| Na. | Aina ya Biashara | Kiwango kwa Mwezi |
|---|---|---|
| 1. | Pombe za kienyeji | 2,000 |
| 2. | Maduka ya rejareja | 5,000 |
| 3. | Mama, baba lishe | 1,000 |
| 4. | Ghala za mbao | 10,000 |
| 5. | Restaurant (mgahawa) | 3,000 |
| 6. | Maduka ya jumla | 5,000 |
| 7. | Nyumba za kulala wageni | 5,000 |
| 8. | Mashine za kusaga | 4,000 |
| 9. | Viwanda vya mikate | 3,000 |
| 10. | Mashine za kuranda mbao | 5,000 |
| 11. | Ofisi za Sekta binafsi | 2,000 |
| 12. | Baa zote za pombe za kigeni /grocery | 5,000 |
| 13. | Viwanda vya useremala | 2,000 |
| 14. | Saloon/vinyozi | 10,000 |
| 15. | Gereji ya magari/pikipiki | 20,000 |
| 16. | Kuchoma mahindi` | 1,000/= |
| 17. | Wauza barafu | 1,000/= |
| 18. | Maduka ya nyama | 5,000 |
| 19. | Workshop welding | 5,000 |
| 20. | Watengenezaji wakubwa wa barafu | 3,000 |
| 21 | Wauza mkaa jumla | 3,000 |
| 22. | Wauza mkaa reja reja | 1,000 |
| 23. | Filing station | 10,000 |
| 24. | Zahanati binafsi | 10,000 |
| 25. | Hospitali/vituo vya afya binafsi | 300,000 |
| 26. | Biashara ndogo ndogo zisizotajwa | 1000 |
| 27. | Ghala | 10,000 |
| 28. | Viwanda | 20,000 |
| 29. | Shule/vyuo binafsi | 5,000 |
| 30. | Mafundi cherehani | 1,000 |
| 31. | Vizimba sokoni (kila kimoja) | 1,000 |
| 32 | Kumbi za starehe | 10,000 |
| 33 | Vibanda vya simu | 2,000 |
| 34 | Wauzaji wa ngozi | 10,000 |
| 35. | Kila Kaya | 1,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 222 (Linaendelea.)*

SEHEMU B
ADA YA KUTUPA TAKA KWENYE DAMPO

| NA. | Jina la Kampuni/Viwanda | Ada kwa mwezi | Ada kwa mwaka |
|---|---|---|---|
| 1 | Makampuni ya simu | 30,000 | 300,000 |
| 2 | Taasisi za kifedha | 30,000 | 300,000 |
| 3 | Kampuni nyingine yoyote yenye shughuli zinazozalisha taka. | 100,000 | 1,200,000 |

JEDWALI LA PILI

(*Limetengenezwa chini ya kifungu cha 16)*

KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya ................................ kwamba Tarehe ………Mwezi………...Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo za Usafi wa Mazingira Halmashauri za Wilaya ya Bagamoyo za mwaka 2022.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi elfu thelathini na kutekeleza wajibu niliopewa na Sheria Ndogo hizi badala ya kushtakiwa mahakamanni.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………. ya Mwezi……………..………. Mwaka…………………

Jina………………………………………Saini……………………………………

Mbele ya:

Jina……………………………………...Cheo…………………………………….

Saini……………………………………Tarehe……………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kilichofanyika tarehe 17/11/2021.

SHAURI SELENDA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bagamoyo.*

MOHAMED ABDALLAH USINGA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bagamoyo.*

**L.S**

NAKUBALI,

Dodoma,
1 Machi, 2022

INNOCENT L. BASHUNGWA (MB.),
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi,*